# MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA
# JARIDA LA MTANDAONI
## Ziara ya Bodi ya Wakurugenzi ya NHIF

NATIONAL HEALTH INSURANCE FUND
NHIF
Dedicated to providing quality health Care
ISO 9001:2015 CERTIFIED






# NHIF ILIOKOA MAISHA YA MWANANGU-RAS TABORA
### Tabora





## Awataka Wananchi Kujiunga ili kuwa na Uhakika wa Matibabu

Katibu Tawala wa Mkoa wa Tabora Bw. Rogath John Mboya ameahidi kushirikiana na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), katika kuhamasisha kujiunga na huduma zake ili wajihakikishie huduma za matibabu wakati wote bila kikwazo cha fedha.

Amesema kuwa ameshuhudia NHIF ikiokoa maisha ya mtoto wake wakati alipopatwa na maradhi yaliyohitaji uchunguzi wa kitaalam na wenye gharama kubwa.

Hayo aliyasema wiki hii wakati akizungumza na Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya NHIF katika Ofisi za Mkuu wa Mkoa wa Tabora ambapo Bodi hiyo ilifika ofisini hapo kwa lengo la kuweka mikakati ya mashirikiano ya utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote na kuimarisha mahusiano.

“Suala la kuwa na Bima ya Afya ni suala muhimu kwa wananchi wote na kama hujapatwa na changamoto kubwa za maradhi huwezi kuelewa umuhimu wake, binafsi nimeona NHIF ikiokoa uhai wa mwanangu hivyo tuko tayari kuhakikisha wananchi wanapata elimu na kujiunga,” alisema Bw. Mboya.

Alisema kuwa mchango wa NHIF katika sekta ya afya ni mkubwa hivyo akaupongeza uongozi wa Mfuko kupitia Mkurugenzi Mkuu Dkt. Irene Isaka kwa jitihada kubwa za maboresho yaliyofanyika katika huduma zake ambapo kwa sasa mwanachama anapata huduma kwa urahisi na kwa ubora mkubwa.

Kwa upande wa Bodi ya Wakurugenzi iliyoongozwa na Kaimu Mwenyekiti Bi. Zubeda Chande aliushukuru uongozi wa Serikali ya Mkoa wa Tabora kwa kukubali kushirikiana na NHIF katika kuhakikisha suala la Bima ya Afya kwa Wote linatekelezeka na ndoto ya Serikali ya kila mwananchi kuwa na bima ya afya inakuwa halisi.

“Kipaumbele chetu kama Bodi ni kuona maelekezo ya Serikali yanatekelezwa ili kila mwananchi aweze kunufaika na uwekezaji uliofanyika katika sekta ya afya kwa kupata huduma za matibabu kupitia mfumo wa bima ya afya hivyo tunashukuru sana kwa kuwa tayari kushirikiana na sisi katika hili,” alisema Bi. Chande.



Naye Mkurugenzi Mkuu Dkt. Isaka alitumia fursa hiyo kuwahakikishia wananchi upatikanaji wa huduma bora za matibabu na akaahidi kuendelea kufanya maboresho ya kihuduma ili wananchi waweze kuzifikia huduma za Mfuko ikiwemo usajili na matibabu kwa urahisi zaidi.

Wajumbe wa Bodi walioshiriki ziara hiyo ni Bw. Shabaan Kabunga na Bw. Amour Amour ambaye pia ni Mkurugenzi wa Mipango Wizara ya Afya.








# TUACHE UTENDAJI KAZI WA MAZOEA- BODI NHIF

## Shinyanga





Na Grace Michael, Shinyanga

Bodi ya Wakurugenzi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), imewataka Watumishi kuachana na utendaji kazi wa mazoea na badala yake wajielekeze kwenye utendaji kazi wenye matokeo na unaozingatia utoaji bora wa huduma kwa wanachama wake.

Agizo hilo limetolewa wiki hii katika mikoa ya Shinyanga na Tabora na Kaimu Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Bi. Zuena Chande wakati alipozungumza na Watumishi wa NHIF mikoani humo.

Alisema kuwa katika kipindi hiki ambacho Serikali ina matarajio makubwa na NHIF katika kuwafikia wananchi wote kupitia Bima ya Afya kwa Wote, ni lazima kila Mtumishi abadili mtazamo wake katika kazi ili kuweza kufanikisha malengo yaliyowekwa.


Bi. Chande aliwataka watumishi kuhakikisha wanafanya kazi kwa bidii, maarifa, uadilifu na ubunifu unaohusisha uelimishaji unaotumia njia sahihi katika eneo husika kwa kuzingatia utamaduni na shughuli za kiuchumi za eneo hilo ili kuwezesha kufikisha elimu tarajiwa kwa haraka na kupata mapokeo Chanya.

“Niwaombe sana tukikutana na changamoto yoyote iliyoko nje ya uwezo wenu iwasilisheni kwa Menejimenti ili iwasadie kuitatua na inaposhindwa sisi Bodi tupo kuhakikisha tunafanyia kazi ili msikwame katika kuwafikia na kuwahudumia wananchi,” alisema Bi. Chande.

Kwa upande wake Mjumbe wa Bodi Bw. Amour Amour aliwataka Watumishi kuweka mikakati itakayowezesha utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote ili kutimiza azma ya Serikali ya wananchi wote kuwa ndani ya Mfumo wa Bima ya Afya.

Wakielezea mikakati waliyoiweka Mameneja wa Mkoa wa Tabora na Shinyanga, wameihakikishia Bodi kuwa wamejipanga kuwasikia wananchi wa ngazi za chini zaidi kwa kushirikiana na Watendaji wa Serikali za vijiji, Wahudumu wa Afya na Mawakala waliosajiliwa na Mfuko kusajili wananchi.













Kwa upande wa Mkurugenzi Mkuu Dkt. Irene Isaka, alisema kuwa kazi kubwa iliyoko mbele yake ni kutekeleza maelekezo ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Mhe. Samia Suluhu Hassan ya kuwasajili wananchi ili waweze kupata huduma za matibabu kupitia mfumo wa bima ya afya.

Dkt. Isaka alisisiza utoaji wa huduma bora kwa wanachama unaozingatia maadili na Weledi kwa kuwa huduma zinazotolewa na Mfuko zinahusisha maisha au uhai wa wanachama.

Ziara hii ni mwendelezo wa Ziara zinazofanywa na Bodi ya Wakurugenzi kwa lengo la kupata mrejesho wa huduma na kujionea mazingira ya kazi waliyonayo Watumishi pamoja na kutatua kero wanazokutana nazo katika kuwahudumia wanachama.

**Bima ya Afya kwa Wote, Jiunge Sasa**

# NITAONGOZANA NA NHIF KUHAMASISHA WANANCHI- RC SIMIYU

Na Mwandishi Wetu, Simiyu

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu Mhe.Anamringi Macha amesema yuko tayari kuongozana na Maofisa wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), kwenda kutoa elimu kwa wananchi ili wajiunge na bima ya afya.

Amesema kuwa ili kuepukana na gharama kubwa za matibabu zinazosababisha wananchi kuingia kwenye umasikini na wakati mwingine kupoteza maisha ni kujiunga na bima ya afya ambayo inawezesha kupata matibabu bila kikwazo cha fedha.

Ahadi hiyo ameitoa mbele ya Bodi ya Wakurugenzi ya NHIF iliyotembelea ofisini kwake kwa ajili ya kuweka mikakati ya kuwafikia wananchi wakati wa utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote pamoja na kuimarisha mahusiano ya Serikali ya Mkoa na NHIF.

Alisema kuwa changamoto kubwa iliyopo kwa upande wa wananchi wa Simiyu ni uelewa wa dhana ya bima ya afya hivyo akaahidi kuongozana na Maofisa wa NHIF kwenye mikutano mbalimbali ya wananchi ili watoe elimu ba kuhamasisha.




“Wananchi wa hapa uwezo wa kujiunga na bima ya afya wanao isipokuwa uelewa wa bima ya afya uko chini sana hivyo ni lazima tuwe na mkakati wa kukuza uelewa ili wananchi wajiunge ili wawe na uhakika wa kupata huduma za matibabu bila kikwazo cha fedha,” alisema Mhe. Macha.

Alisema kuwa njia nyingine itakayowezesha ushawishi wa wananchi kujiunga ni pamoja na kuzingatia tamaduni za wananchi wa Simiyu ili kuwezesha mapokeo chanya.

Mhe. Macha alitumia fursa hiyo kuupongeza uongozi wa NHIF kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhakikisha

malengo ya Serikali ya kila mwananchi kuwa na bima ya afya yanafikiwa.

Kwa upande wa Bodi ya NHIF, iliyoongozwa na Kaimu Mwenyekiti Bi. Zubeda Chande aliushukuru uongozi wa Serikali ya Mkoa wa Simiyu kwa kukubali kushiriki katika uhamasishaji na utoaji wa elimu kwa wananchi ili waweza kujiunga na bima ya afya.

Akitoa maelezo ya awali, Mkurugenzi Mkuu wa NHIF Dkt. Irene Isaka alisema kuwa Mfuko umeweka mikakati mingi ya kuwafikia wananchi ikiwemo kutumia mawakala kusajili wananchi.

"Serikali yetu ina matarajio makubwa sana katika utekelezaji wa Bima ya Afya kWa Wote hivyo tutahakikisha tunatumia mbinu zote ikiwemo kubotesha huduma ili wananchi wajiunge na wafurahie huduma," alisema Dkt. Isaka.

Ziara ya Bodi katika mikoa ya Tabora, Shinyanga na Simiyu imelenga kuimarisha mahusiano na kuweka mikakati thabiti ya kuwafikia wananchi katika maeneo yao na kuwahamasisha kujiunga na NHIF.




















# BIMA YA AFYA KWA WOTE KUONDOA CHANGAMOTO ZA MATIBABU- RC MARA

Na Mwandishi Wetu, Mara

Mkuu wa Mkoa wa Mara Mhe. Kanali Evance Mtambi amesema kuwa kuanza utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote kutasaidia kuondoa changamoto za huduma za matibabu kwa makundi yote ya wananchi.

Kutokana na hilo ameutaka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kuendelea kuimarisha Mifumo yake ikiwemo ya utambuzi na udhibiti wa vitendo vyenye viashiria vya udanganyifu ili uhai na uhimilivu wa Mfuko uendelee kuimarika.

Haya aliyasema wiki hii ofisini kwake wakati akizungumza na Bodi ya Wakurugenzi ya NHIF iliyofika ofisini hapo kwa lengo la kuweka mikakati ya ushirikiano katika utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote ili wananchi waweze kujiunga na kuwa na uhakika wa huduma za matibabu wakati wote.

"Uwepo wa Bima ya Afya kwa Wote utasaidia makundi yote yakiwemo ya Wazee, watoto, walemavu na makundi mengine kunufaika na huduma za matibabu kupitia mfumo wa bima ya afya," alisema Mhe. Kanali Mtambi.

Kutokana na hayo alitoa rai kwa NHIF kuongeza wigo wa utoaji wa elimu kwa wananchi hususan wa maeneo ya vijijini ili wafahamu umuhimu wake

na wachukue hatua ya kujiunga.

Kwa upande wa Ofisi ya Mkoa, aliuhakikishia Mfuko ushirikiano katika utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote ili lengo la kila mwananchi kuwa ndani ya mfumo wa bima ya afya litimie.

Akizungumzia utayari wa utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote, Mkurugenzi Mkuu wa NHIF Dkt. Irene Isaka alisema maandalizi makubwa yaliyofanywa ni pamoja na maboresho ya mifumo ambayo inasomana na taasisi zingine kwa ajili ya kupata taarifa za wanachama kwa haraka.

"Mifumo yetu kwa sasa inasomana na inatuwezesha kupata taarifa za mwanachama wakati anapopata huduma hospitali na inasaidia kwa kiwango kikubwa kudhibiti vitendo vya udanganyifu" alisema Dkt. Isaka.

Kwa upande wa Bodi ya Wakurugenzi iliyoongozwa na Dkt. Zubeda Chande alisema Mfuko utaendelea na uboreshaji wa huduma kwa kuzingatia uhai na uhimilivu wa Mfuko ili uendelee kuwa imara na kutoa huduma bora.

Alisema kuwa mrejesho unaopatikana kupitia wanachama, wananchi na viongozi wa serikali unasaidia katika kufanya maboresho na kutatua changamoto zinazohitokeza katika huduma.

"Tunashukuru sana kwa ushirikiano ambao mnatupatia kupitia Ofisi yako ili kufanikisha utekelezaji wa shughuli zetu, kazi kubwa iliyoko mbele yetu ni kuwafikia wananchi na wajiunge ili wapate huduma wanapozitaka," alisema Dkt. Chande.




















# MTANDAO WA NHIF KUWAFIKIA WANANCHI WOTE













Na Mwandishi Wetu, Mwanza

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), umetajwa kuwa ni Mfuko wenye mtandao mkubwa unaoweza kufanikisha utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote kwa kuwafikia na kuwasajili wananchi kwenye mfumo wa bima ya afya.

Mtandao huo utatumika kufikisha elimu ya dhana ya bima ya afya, uhamasishaji wa wananchi na usajili wa wanachama wakati wa utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote.

Hayo aliyasema wiki hii Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza Bw. Balandya Elikana wakati akizungumza na Bodi ya Wakurugenzi ya NHIF ofisini kwake ambayo ilifika kwa lengo la kuweka mkakati wa kuwafikia wananchi na kupata mrejesho wa huduma kwa lengo la kuboresha zaidi.

Akizungumzia namna ya kuwafikia wananchi, aliutaka Mfuko kuangalia uwezekano wa kuwawezesha wananchi wote kujiunga kupitia vifurushi mbalimbali ili waweze kuchagua na kujiunga ili kuwa na uhakika wa huduma za matibabu wakati wanapozihitaji.

"Bima ya Afya kwa Wote ndio mkombozi wa wa wananchi katika kupata huduma za matibabu hivyo naamini kupitia mtandao wenu mkubwa hapa nchini mtaweza kuwafikia wananchi wote ili kutimiza lengo la Serikali la wananchi kupata huduma bora kupitia bima ya afya" alisema Bw. Elikana.

Alisema kuwa endapo wananchi watafikiwa na kujiunga itawasaidia kuwa na uhakika wa kupanga na kushiriki kikamilifu shughuli za maendeleo na hatimaye kukuza uchumi wao na wa Taifa kwa ujumla.

"Hakuna mbadala wa bima ya afya kwa kuwa ndio njia pekee inayomwezesha mwananchi kuwa na uhakika wa kupata huduma za matibabu bila kikwazo chochote na kwa uwekezaji uliofanyika kwenye sekta ya afya umewezesha upatikanaji wa huduma bora na zenye uhakika," alisema.

Akizungumzia mikakati ya kuwafikia wananchi, Mkurugenzi Mkuu wa NHIF Dkt. Irene Isaka alisema kuwa Mfuko umejioanga katika maeneo yote kuhakikisha wananchi wanafikiwa na kusajiliwa.

"Tunaendelea na utoaji wa elimu na kuhamasisha wananchi kujiunga kupitia vifurushi mbalimbali lakini pia tumeendelea kuboresha uoatikanaji wanhuduma," alisema Dkt. Isaka.

Akitoa salaam za Bodi Kaimu Mwenyekiti wa Bodi Dkt. Zubeda Chande alisema kuwa Mfuko utaendelea kushirikiana na Ofisi ya Serikali ya Mkoa katika kuwafikia wananchi na kutimiza ndoto ya Serikali.
Bima ya Afya kwa Wote, Jiunge Sasa






# NHIF TUMIENI FURSA GEITA- MHE. SHIGELA





Na Mwandishi Wetu, Geita

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), umeombwa kutumia fursa za uwepo wa vyama vya wachimbaji madini mkoani Geita kwa lengo la kuongeza wigo wa wanachama hususan katika kipindi hiki cha utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote.

Rai hiyo imetolewa wiki hii na Mkuu wa Mkoa wa Geita Mhe. Martin Shigela wakati alipozungumza na Bodi ya Wakurugenzi ya NHIF iliyoongozwa na Kaimu Mwenyekiti Dkt. Zubeda Chande.

Alisema kuwa Mkoa wa Geita unazo fursa nyingi kutokana na shughuli kubwa za kiuchumi zinazoendelea mkoani hapo ambazo zinawawezesha wananchi kumudu gharama za kujiunga na bima ya afya na kuwa na uhakika wa matibabu wakati wote.

"Hapa tunavyo vyama vya wachimbaji wadogo wadogo ambao wana uwezo wa kifedha kulipia gharama za kujiunga hivyo wekeni mikakati ili tushirikiane kwa pamoja kuwafikia na kuwapa elimu ya umuhimu wa kuwa ndani ya mfumo wa bima ya afya," alisema Mhe. Shigela.

Alisema kuwa NHIF ni nguzo kubwa katika ustawi wa jamii hivyo ni wajibu kuhakikisha wananchi wanafikiwa na wanahamasishwa kujiunga na hatimaye kuwa na uhakika wa kupata huduma za matibabu bila kikwazo cha fedha.

Katika hatua nyingine alipongeza Mfuko kwa kazi kubwa inayofanya ya kuwahudumia watanzania na akaahidi ofisi yake iko tayari kushirikiana katika kutoa elimu lakini pia kusimamia huduma zinazotolewa na watoa huduma ili ziwe bora zaidi na kuvutia zaidi wananchi kujiunga na NHIF.

Kwa upande wake Dkt. Chande kwa niaba ya Bodi, alishukuru Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa ushirikiano inaotoa kwa Mfuko, unaowezesha kuwafikia wananchi kwa urahisi hatimaye kuwezesha utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote.

"Tunafarijika sana kama Bodi tunapopata mrejesho kama huu kutoka kwenu viongozi, tunaamini hata utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote utakuwa wenye ufanisi zaidi na tutatimiza ndoto ya Serikali ya kila mwananchi kuwa na Bima ya Afya," alisema Dkt. Chande.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Dkt. Irene Isaka alimhakikishia Mkuu wa Mkoa kuwa Mfuko uko tayari na umejipanga kuhudumia wananchi wengi zaidi ambapo umefanikiwa kufanya maboresho ya Mifumo inayowezesha kutoa huduma kwa ufanisi mkubwa lakini pia maboresho katika huduma za matibabu ambazo zimezingatia mahitaji halisi na gharama nafuu.

"Tunashukuru sana kwa kutuonesha fursa zilizopo hapa, mimi na wenzangu tutalifanyia kazi kwa haraka kwa kuja kukutana na vyama hivi lakini pia Watoa huduma kuona mahitaji yao ya maboresho ili waweze kutumia fursa ya Mikopo ya Vifaa tiba, TEHAMA, dawa na ukarabati wa miundombinu na hii inasaidia kuboresha huduma kwa ajili ya wanachama wetu na wananchi kwa ujumla," alisema Dkt. Isaka.




# TUMIENI FURSA ZA KIUCHUMI GEITA KUSAJILI WANACHAMA- BODI NHIF







Na Mwandishi Wetu, Geita

Bodi ya Wakurugenzi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), imeiagiza Ofisi ya Mkoa wa Geita kutumia fursa zilizopo mkoani humo kuwahamasisha wananchi kujiunga na bima ya afya ili wawe na uhakika wa kupata huduma za matibabu.

Agizo hilo limetolewa wiki hii na Kaimu Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Dkt. Zubeda Chande wakati akizungumza na Watumishi wa NHIF Mkoa wa Geita muda mfupi baada ya kuwa na kikao na Mkuu wa Mkoa huo Mhe. Martin Shigela.

Alisema kuwa Mkoa wa Gaita unazo fursa nyingi kutokana na uwepo wa shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwemo uchimbaji wa madini, uvuvi, Kilimo na biashara. Shughuli ambazo zinawezesha wananchi kuwa na kipato cha kugharamia mahitaji ikiwemo bima ya afya.

“Tumetoka kukutana na Mkuu wa Mkoa, ametueleza namna Mkoa ulivyo na fursa nyingi ikiwemo wananchi wake kuwa na uwezo wa kugharamia bima ya afya, nawaagiza kuweka mikakati yenu vizuri ili kuwafikia wananchi hawa kwa makundi. Nahimiza huduma bora kwa wanachama. Muweke usimamizi mzuri wa vituo tulivyovisajili ili tuweze kuvutia wananchi wengi na kuondokana na malalamiko” alisema Dkt. Chande.

Naye Mjumbe wa Bodi Wakili. Shaban Kabunga aliwataka Watumishi kuwa na malengo mahsusi yanayoweza kuleta matokeo katika usajili wa wanachama na ukusanyaji wa michango. Aliwataka kutumia takwimu kubainisha wadau na fursa zilizopo ili kuwezesha usajili wa wananchi.

Naye Bw. Amour Amour ambaye ni Mjumbe wa Bodi na Mkurugenzi wa Mipango Wizara ya Afya, aliwataka Watumishi kuhakikisha wanasimamia ubora wa huduma zinazotolewa kwa wanachama na Vituo vya kutolea huduma ili kuwezesha kuvutia wananchi wengine kujiunga na bima ya afya. Alisema Sera ya Afya imejikita kwenye uboreshaji wa huduma za Afya hivyo kupitia Sera pamoja na Sheria ya Bima ya Afya kwa wote ni fursa nzuri kwa NHIF kuongeza wigo wa wanachama.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Dkt. Irene Isaka alisisitiza utendaji kazi unaozingatia maadili ya utumishi wa umma, ubunifu pamoja na kufuata Sheria, Kanuni, taratibu na miongozo iliyopo ili kuepukana na malalamiko na kuongeza ufanisi.

Alitumia fursa hiyo kuwakumbusha Watumishi hao kuhamasisha vituo vya Afya kuhusu uwepo wa fursa za Mikopo ya vifaa tiba, dawa na ukarabati wa majengo unaolenga kuboresha huduma katika vituo vilivyosajiliwa na Mfuko.

“Tuvipitie vituo vyetu na kuangalia maeneo wanayoweza kuboresha kupitia mikopo yetu nafuu ili kuwezesha kutoa huduma bora zaidi kwa wanachama na wananchi kwa ujumla,” alisema Dkt. Isaka.

Naye Meneja wa Mkoa wa Geita Bw. Odhiambo, aliihakikishia Bodi kutekeleza maagizo ya Bodi ikiwemo kukutana na vyama vya wachimbaji wadogo wadogo wa madini ambao wana uwezo mkubwa wa kifedha wa kulipia bima ya afya.

**BIMA YA AFYA KWA WOTE, JIUNGE SASA**






# WEKENI MKAZO KWENYE UTOAJI WA ELIMU- BODI NHIF







Na Mwandishi Wetu, Kagera

Bodi ya Wakurugenzi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), imeziagiza Ofisi zote za Mfuko kuweka mkazo katika utoaji wa elimu ya bima ya afya kwa wananchi ili wafahamu manufaa yake hatua itakayowezesha kujiunga na kuongeza idadi ya wanachama.

Agizo hilo limetolewa wiki hii na Kaimu Mwenyekiti wa Bodi Dkt. Zubeda Chande wakati wa hitimisho la ziara ya Bodi hiyo katika mikoa ya Tabora, Shinyanga, Simiyu, Mara, Mwanza, Geita na Kagera. Dkt. Chande ameongozana na Wajumbe wa Bodi Bw. Amour Amour na Bw. Shaban Kabunga.

Katika ziara hiyo, Bodi ya NHIF imefanikiwa kukutana na Wakuu wa Mikoa na kuweka mikakati ya kuwafikia wananchi katika utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote, kupata mrejesho wa huduma toka kwa wanachama na kuimarisha mahusiano ya Mfuko na Serikali za Mikoa.

Alisema kuwa katika kipindi hiki ambacho Serikali inataka wananchi wake wawe na bima ya afya, ni vyema kila ofisi ikaongeza kasi ya utoaji wa elimu kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo njia zinazohusisha utamaduni wa mkoa husika ili kurahisisha ufikishaji wa elimu hiyo.

"Serikali inatuangalia na inahitaji tuwafikie wananchi na kuwasajili ili wawe na uhakika wa kupata huduma za matibabu bila kikwazo cha fedha, kwa upande wake Serikali imefanya kazi kubwa ya kuwekeza katika vituo kwa kuweka vifaa tiba vya kisasa, dawa na miundombinu hivyo kinachotakiwa ni sisi kuwafikia wananchi na kuwasajili ili wanufaike na huduma hizo," alisema Dkt. Chande.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Dkt. Isaka aliwataka Watumishi kila mmoja kwa nafasi yake kuhakikisha anajituma kutokana na malengo yaliyowekwa ili kufanikisha matamanio ya Serikali.

"Kwa Watumishi wote hususan mlioko huku mikoani, nawaomba sote tuwe na mtazamo chanya wa kuwepo huku kwa kuwa tumeaminiwa kuwahudumia wananchi hivyo kila mmoja kwa nafasi yake ahakikishe anatekeleza majukumu yake ipasavyo kwa weledi na kwa kuzingatia taratibu na miongozo iliyopo," alisema Dkt. Isaka.

Kwa upande wa Ofisi za Mikoa hiyo, kwa pamoja wameiahidi Bodi kufanya kazi kwa kujituma ili lengo la kuwasajili wananchi katika meneo yote liweze kufikiwa.

Mfuko kwa sasa umesogeza zaidi huduma kwa wananchi kwa kuwa na Ofisi kila Mkoa lakini pia imefanikiwa kufungua Ofisi katika maeneo ya kimkakati ambayo ni pamoja na Ifakara mkoani Morogoro, Karagwe mkoani Kagera, Kahama mkoani Shinyanga, Bukombe mkoani Geita, Tegeta mkoani Dar es Saalam na Nzega mkoani Tabora. Lengo kubwa la Ofisi hizi ni kusogeza huduma zaidi kwa wananchi na kufanikisha utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote.

**Bima ya Afya kwa Wote, Jiunge Sasa**